LEARNING BY EAR EPISODE – Girls
9th Episode: Careers

Text: Zainab Aziz
Redaktion: Andrea Schmidt/Christine Harjes

CHARACTERS:
Anchor. Intro / Autro
Bibiy......Main Character
Teacher......woman Adult.
Sofia......Same Character in episode 1
Tamara......Same Character in episode 7
Career expert........man Adult.

Intro: Karibu msikilizaji kwenye mchezo wa kuigiza katika makala ya jifunze Kwa Kusikiliza. Leo Bibiy na wenzake wanachagua kazi. Ni wazi kuwa wasichana hawa wanamatumaini makubwa ya kufanya kazi wanazozipenda baada ya kumaliza masomo yao. Je wanatumia vigezo gani kufanikisha lengo lao. Karibu kwenye sehemu ya tisa ya mchezo kwa jina Kuchagua Kazi.

Sign Tune.......

SCENE ONE

(Darasani wasichana wanazungumza)

TEACHER: Shhh!!!! ...tafadhalini.. hebu nyamazeni kimya (Sauti zinafifia) ... Nina furaha tele kuwajulisheni kuwa leo tutatembelewa na mgeni ambae ni mtaalamu wa maswala ya kazi , mtalaam huyo atakuja hapa kuzungumza nanyi kuhusu njia za kuchagua kazi. Mazungumzo ya leo yanalenga kuwanoa mawazo yenu ili mtakapo kuwa tayari kuchagua ni kazi gani kila mmoja wenu angetaka kufanya muwe mna ujuzi wakutosha.Nina hakika kila mmoja wenu hapa anataka kuwa mtu fulani au anataka kufanya kazi fulani katika maisha yenu ya

usoni baada ya kumaliza masomo, kwa hivyo basi ninatarajia mtauliza maswali mengi kwa manufaa yenu

SOFIA: mwalimu nauliza kama kwanza tunaweza kujadiliana sisi wenyewe kabla ya mtalaamu huyo kufika?

TEACHER: Ndio inawezekana Sofia ... enhee wewe unasemaje hebu tuambie ni ipi ndoto yako kuhusu kazi baada ya kumaliza masomo?

SOFIA: Mimi mwalimu ningependa kuwa mwanasiasa, hivi ninafanya bidii kwenye masomo yangu kwani ninahitaji kwenda chuo kikuu ili ndoto yangu niikamilishe..baada ya matatizo yaliyonipata kutokana na baba yangu kutaka kuniozesha kwa mzee mmoja tajiri..nimejifunza mengi hasa baada ya kufaulu kugeuza nia ya baba yangu kwa msaada wenu.. sasa mimi ni msichana mwenye mtazamo tafauti kabisa nataka kusoma baadae niwatetee raia.

TEACHER: Vizuri sana Sofia ... ni muhimu sana kusoma kwa bidii namimi nakusisitiza uendeleze bidii hiyo ili ufanikiwe..najua unaweza...mnaona kuwawezesha wasichana ni jambo la muhimu sana tena linaleta faida kubwa katika jamii hakika wasichana wakiwezeshwa wanaweza kuleta mabadiliko mengi yenye manufaa katika jamii..Enhee!!..na wewe Tamara unataka kufanya kazi gani?

TAMARA: Mimi mwalimu ndoto yangu ni kuwa daktari kwa kuwa ninataka kuwasaidia wagonjwa.

TEACHER: Vyema sana..kwa kweli kinachomtia mtu changamoto hadi akachagua kazi ya aina hii, ni kwa sababu ya ile hamu kubwa ya kutaka kuponya maisha na kufanikisha hilo lazima pia ufanye bidii kubwa katika masomo yako...narudia ni lazima mjibidiishe kwani hakuna mtu atakae wasomea..naona sasa mgeni wetu amefika na hebu tumkaribishe kwa makofi.

(Wasichana wanapiga makofi)

EXPERT: Asanteni sana kwa makaribisho..naam jina langu naitwa Bob na mie ni mtalaamu wa maswala ya kuchagua kazi..naamini kuwa jambo hili linawafurahisha sana vijana..nami nashukuru kwa kupata fursa kama hii ya kuweza kuzungumza na wasichana kuhusu mipango yenu ya baadae kuhusiana na maswala ya kuchagua kazi hivyo basi natumai tutakuwa na siku yenye mafanikio makubwa.

(Kengele inalia)

TEACHER: kengele ndio hiyo imelia na sasa ni wakati wa mapumziko..tutaendelea na mazungumzo yetu baadae.mnaweza kutoka nje.

MUSIC...........

SCENE TWO:

SOFIA: Vipi Bibiy.. Nimefurahi sana kukuona..mambo vipi?

BIBIY: ooh Sofia ...hata nami nimefurahi sana kukuona..mimi ni mzima sina neno. Hee hongera sana rafiki yangu nimepata habari kuwa umepata tena zawadi ya mwananfunzi bora..kwa kweli hiyo iantia moyo sana..enhee na vipi baba yako hajambo mambo yanaendeleaje Sofia?

SOFIA: Yeah! ... Bibiy kila kitu ni sawa kabisa nashukuru kuwa hata baba yangu amebadilika kweli kweli yaani amekuwa mtu tofauti kabisa. Baba yangu siku hizi yuko mstari wa mbele katika kuunga mkono maswala ya elimu nakwambia Bibiy hivi sasa anawasaidia wasichana wawili kutoka familia masikini anawalipia karo ili waendelee na masomo yao.. Ooh!! Jambo la kufurahisha ni kuwa baba yangu ameendelea sana tangu afungue duka la vitabu .. Bibiy rafiki yangu sitakusahau kwamwe..inabidi uje siku moja umtembelee baba yangu.

BIBIY: Bila shaka Sophia nitamuomba nyanya yangu ruhusa

akikubali pia naweza kuja nae kwenu..loo nimefurahi sana kusikia habari hizo njema.. Hey Sophia samahani rafiki yangu itanibidi nikuache sasa kwani ninaelekea ofisini kwa mwalimu mkuu, ninataka kumuarifu kuhusu msichana mmoja ambae amenyimwa fursa ya kuja shule anafanya kazi kwenye eneo la ujenzi..masikini anabeba mifuko ya simenti na hata ndoo za mchanga nilipomuuliza akaniambia kuwa inambidi afanye kazi hiyo ili kumsaidia mama yake mgonjwa.

SOFIA: Mimi nashindwa kuelewa jamani kwanini wasichana wanyimwe fursa ya kwenda shule? Kwa nini wafanye kazi ngumu kwa ajili ya kuzitunza familia? Bibiy nakutegemea sana najua utamsaidia msichana huyu kama kawaida yako.

BIBIY: Ooh Sofia hilo ndilo lengo hasa la kikundi chetu cha Girl Power..nia na madhumuni yetu ni kuangazia maswala mbali mbali yanayotukabili sisi wasichana..tunataka kuzimulika shida mbali mabli na hatimae kuzitafutia ufumbuzi. Namshukuru sana nyanya yangu kwa ushauri wake.

SOFIA: Hata mimi nitamueleza baba yangu kuhusu msichana huyo, natumai ataweza kumsaidia ili arejee shuleni ...ninasikitika sana ninaposikia wasichana wanataabika hadi kushindwa kwenda shule (kengele inalia) ... Ooh Bibiy kwaheri kengele imelia ninarudi darasani..nakutakia kila la kheri.

BIBIY: ..Asante sana Sofie...nisalimie wote.

African Drums

SCENE THREE:

TEACHER: Naam wasichana bila shaka sasa tuko tayari kuendelea na mazungumzo yetu, mgeni wetu bwana Bob nae yuko tayari kabisa kuzungumza nasi..karibu sana mtaalamu wetu.

EXPERT: Nashukuru .. Thank you ... naam ninafuraha kuwa

nanyi tena wasichana na moja kwa moja nitaanza mazungumzo yetu kwa kuwaambia kuwa huu ndio wakati muafaka kwenu kuanza kufikiria juu ya kazi ambazo mngependa kuzifanya baada ya kumaliza masomo yenu..wakati wa mapumziko mwalimu hapa amenieleza kazi ambazo baadhi yenu mngependa kuzifanya na kwa kweli nimevutiwa sana nataka mfahamau kuwa ni sawa kabisa kwenu kuanza kufikiria juu ya kazi hivi sasa lakini yote hayo yatawezekana tu ikiwa mtajifunza mbinu za kufikiria na kutekeleza mawazo yenu.

TAMARA: Lakini vipi tunaweza kutambua juu kazi tunazotaka kuzifanya tukimaliza masomo yetu ili hali wengi wetu hatuwezi kufafanua mawazo yetu? Hasa tukizingatia kuwa kazi nyingi zinafanywa na wanume tu je tutafanyaje ili nasi wasichana tuweze kuzifanya kazi hizo pia?

EXPERT: Hilo ni swali zuri sana ..kwanza ni kama nilivyosema hapo awali kuwa wasichana mnahitaji maelezo sahihi kuhusu kazi pia mnahitaji kuondoa kabisa uoga juu ya kufanya kazi ambazo kwa kiwango kikubwa zinafanywa na wanaume..zimepitwa na wakati siku zile ambapo ni wavulana tu ndio waliokuwa na ndoto ya kuwa marubani, wanaanga au hata wahandisi kinachohitajika ni msichana kujibidiisha katika masomo ya hisabati, sayansi na teknolojia pamoja na masomo mengine yote..ili naye awe na uwezo wa kushindana katia soko la ajira.

SOFIA: Ningependa kujua tufanyeje ili kujua ni kazi gani zitakazo tufaa baada ya masomo yetu? Nadhani wengi wetu tuna tatizo hilo.

EXPERT: kwanza jijue wewe mwenyewe, utambue ni masomo gani unayo yapenda zaidi halafu wafikirie watu wawili au watatu ambao unaona kuwa ni kielelezo kwako..jiulize watu hao wanafanya nini?..pia jaribu kujua wamefanyaje ili kufikia pale walipo..ni muhimu pia kujua yanayohitajika ili kufikia uwezo wa kufanya kazi kama wanayofanya watu hao...nadhani ukiyatilia hayo maanani yatakuwa ndio chanzo cha kukupa faraja kubwa

moyoni na kufungua upeo wa mawazo yako kwa jumla..pia msisahau kuwa mnaweza kutafiti kwenye mtandao kuhusu websites zenye kutoa maelekezo juu ya maswala mbali mbali kuhusu kazi pamoja na mahitaji yake.

TEACHER: Labda niongeze hoja, wasichana wanapaswa kuhimizwa kupanuza upeo wa elimu kwa sababu kuna uwiyano kati ya elimu na kazi...yaani kama alivyo sema mtaalamu mnapaswa kujipa nafasi ya kusoma masomo yale ambayo kwa kawaida hamuyapendi, pia mnahitajika kuwasikiliza wenzenu ili kujiongezea ufahamu.

EXPERT: Ukiwa na mbinu kabambe za kufikiria na kutekeleza mawazo yako basi utakuwa mmoja kati ya wanawake wenye ujuzi na elimu hapo baadae, kumbuka kufikia yote hayo lazima uanze sasa. Pia ningependa kusisitiza juu ya kuwa na mtu anayekupa maelekezo maishani.

TAMARA: Je mtu huyo ni nani?

EXPERT: Huyo ni mtu ambae wakati wote anataka kuona maendeleo yako anakupa maelekezo ili ufanikishe malengo yako. Na mtu huyo hapa anaweza kuwa ni mzazi wako, dada yako mkubwa au hata mwalimu wako na kadhalika, uhusiano huu wa muhimu utakuwa na uzito mkubwa katika kuongoza maisha yako.

SOFIA: Je vipi kuhusu kazi inayohusiana na komputa. Je kazi ya aina hii imaweza kweli kuwa ni kazi nzuri kwa wasichana?

EXPERT: Bila shaka kazi inayohusiana na komputa inaweza kuwa ni miongoni mwa kazi bora zaidi kwa wasichana mfano unaweza kuwa muhandisi wa software za komputa au mtaalamu wa mambo ya komputa, pengine hata msimamizi au afisa anaeshughulikia maswala ya mauzo au hata mkurugenzi. Ulimwengu wa sasa unategemea zaidi komputa.

TEACHER: Naam wasichana natumai yale yote tuliyoelezewa

na mataalamu wa kazi bwana Bob yataweza kuwasaidia kujenga mawazo juu ya kazi gani hasa ambazo mgependa kuzifanya baada ya kumaliza masomo yenu..natumai kuanzia sasa kila mmoja wenu ataanza kunoa bongo juu ya kuchagua kazi.

EXPERT: Na mimi nawashukuru sana kwa kunisikiliza na pia kwa kuuliza maswali mengi..mnaweza vilevile kuniuliza mengi wakati wowote mtakapokuwa mnahitaji ufafanuzi, mwalimu atawasidia kufikisha maswali yenu kwangu kwani anuani zangu zote anazo, nami nitayajibu maswali yenu kwa moyo mkunjufu, vinginevyo ninatarajia kukutana nanyi tena baada ya miaka mitano au sita hivi ambapo mtakuwa mmeanza kutekeleza yale tuliyoyazungumza leo hii..nawatakia kila kheri katika kufikia malengo yenu.

(wasichana wanapiga makofi)

TEACHER: Asante sana mtaalamu wetu nasi tunakushukuru kwa kuja hapa na kuzungumza nasi juu ya mada muhimu. Natumai wasichana watayatumia maelezo waliyoyapata kuhusu njia bora za kufikiria na kutekeleza mawazo..hasa wakati huu ambao wanajipanga kuanza kufikiria juu ya kazi watakazozifanya baada ya kumaliza masomo.

MUSIC

SCENE FOUR:

(Wasichana wako njiani wanalekea nyumbani.Ndege wanasikika wakiimba)

SOFIA: Tamara mimi nimependezwa sana na yale tuliyo elezewa na mtaalamu wa kazi leo hii..unajua amenifanya nibadili mawazo yangu ya awali sasa nataka kuwa mtaalamu wa komputa, sitaki tena kuwa mwanasiasa.

TAMARA: Hata mimi alinichota mawazo yangu yote pale

alipozungumzia kuhusu kazi ya udaktari yaani nilidhania alikuwa anazungumza na mimi moja kwa moja..Loo Yule ni mtalaamu kweli kila swali tulilomuuliza alitujibu tena kwa ufasaha..lakini Sofia kwanini unataka kubadili nia yako sasa?

SOFIA: Kwa sababu komputa ndio teknolojia ya kisasa..pia nafikiria kuwa nitakuwa na wakati mzuri sana kufanya kazi katika ulimwengu wa komputa. Kweli Tamara hamu yangu kubwa sasa iko kwenye komputa na wala sio siasa..wewe hukusikia pale mtaalamu aliposema kuwa ulimwengu wa sasa unatagemea komputa? Na mimi sitaki kuachwa nyuma nataka mtaalamu tena wa uhakika.

(Mbwa wanabweka na sauti ya ng'ombe pia inasikika!!)

TAMARA: Hee!! ... Bibiy unakwenda wapi saa hizi?

BIBIY: Hallo Sofia na Tamara ...mimi nakwenda kwa kina Samera sijui kama mnamkumbuka huyo msichana bado?

TAMARA: Yeah!! Tunamkumbuka si ni Yule msichana aliekuwa na matatizo wakati fulani, masikini alipata mimba..tena mjomba wake ndio aliempa hiyo mimba..anaendeleaje sasa..loo ni muda mrefu hatujasikia chochote juu yake.

BIBIY: Hana neno anaendelea vizuri...hata hivi sasa anajitayarisha kurejea tena shule.

SOFIA: Na Yule mjomba wake alifanywa nini? Kesi yake iliishia wapi?

BIBIY: Oooh!!! Nakwambia alipata adhabu inayomsatahili..hivi sasa yuko jela anaipata joto ya jiwe na hatimae rafiki yetu Samera yuko tayari kurejea tena shule ameniambia anatakaa kuwa rubani akimaliza masomo.

TAMARA: hiyo ni habari njema hata hii leo tulitembelewa na mtaaalamu wa kazi shuleni alitueleza mambo mengi tu kuhusu

kuchagua kazi na pia alituhimiza kufikira kufanya kazi ambazo zamani wavulana walifikiria kuwa ni za kwao tu.

BIBIY: Hiyo ni kweli ... hamkumbuki vile tulivyocheza football na kuwashinda wavulana..hawakuamini kuwa tunaweza kuupiga mpira na kuufukuza kwa haraka kushinda wao.

SOFIA: Bibiy lakini mimi nafikiria rafiki yetu Samera alipata matatizo mazito kuliko sisi wote..na wewe umesaidia sana kutatua matatizo hayo.

BIBIY: Ni kweli lakini kila mmoja wetu ametoa mchango mkubwa, binafsi siachi kumshukuru nyanya yangu kwa mawaidha yake mazuri kwa mfano yeye huniambia kuwa haki za wanawake zinaanzia kwa wasichana tena pale wanaposhirikiana kwa mambo mbalimbali..Tamara na Sofia niacheni niendelee na safari yangu tutaonana wakati mwingine.

TAMARA: Ok Bibiy, msalimie sana Samera na umwambie tunafuraha kuwa atarudi shule.

MUSIC

SOFIA: Oooh!! nakwambia Bibiy hata sijui yeye atafanya kazi gani kwa sababu mimi naona yeye ana uwezo wa kufanya kila aina ya kazi natamani ningelikuwa kama yeye!!.

TAMARA: Yeye ni msichana wa aina yake tena ana kipawa cha hali ya juu kisha ana bidii sana.

SOFIA: Watu wengi wanampenda kwa sababu yeye haogopi kusema ukweli, yeye ni jasiri...Tamara hivi unafanya nini baadae leo?

TAMARA: Eenh kwanza nataka kufanya kazi zangu za shule halafu nitakuwa nina muda kwani una mpango gani?

SOFIA: Ninadhani kama utakuwa na nafasi basi twende

tukaangalie basketball timu ya wasichana inachuana na ile ya wavulana leo katika uwanja wa jamii.

TAMARA: Aah kweli!!.kama ni hivyo basi ngoja nitamuomba mama yangu ruhusa halafu baadae nitakupitia nyumbani kwenu twende zetu.

SOFIA: Ok Tamara tutaonana baadae nitakusubiri.

MUSIC.

Autro: Na mpaka hapo ndio ndio tumefikia mwisho wa sehemu hii ya tisa ya mchezo Kuchagua Kazi, wasichana leo hii wamefundishwa jinsi ya kufikiria na kutekeleza mawazo yao. Unaweza kuusikiliza mchezo huu kwa mara nyingine tena au mwambie rafiki yako ausikilize kupitia tovuti yetu www.dw-world.de/lbe hadi tukapokutana tena katika sehemu ya kumi ya makala haya ya Jifunze Kwa Kusikiliza ,kwaherini.

END